SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA

PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA ELIMU

MPANGO WA MAENDELEO YA ELIMU YA MSINGI (MMEM)

(2002 – 2006)

KAMATI YA MAENDELEO YA ELIMU YA MSINGI (BEDC)

Marekebisho
Aprili 2003.

DIBAJI

Wizara ya Elimu na Utamaduni inaanzisha programu kubwa ya maendeleo ya elimu kuhakikisha kwamba kila mtoto atapata elimu nzuri na bora. Mpaka sasa kuna watoto 4,842,875 walioandikishwa tayari katika shule za msingi nchini Tanzania, na kufikia miaka ya 2002 – 2006 kutakuwa na ongezeko la watoto 6,848,692 wenye umri wa kwenda shule watakaoandikishwa.

Hii ni rasilimali kubwa kwa nchi. Kila mmoja katika watoto hawa ana haki yake kipekee ya hisia, mihemko, vipaji, matarajio na uwezo ambavyo vinaweza kuchangia katika maendeleo ya taifa. Ninatambua kwamba kama uwekezaji thabiti utafanywa kwa shauku ya kuelimisha watoto wote na vijana, nchi itakuwa na uhakika wa maisha ya baadaye yenye ustawi.

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ni matokeo ya juhudi za kufasiri Sera ya Elimu na Mafunzo ya Tanzania na malengo ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu, pamoja na malengo ya kimataifa ya Elimu kwa wote (EFA) 2000 katika mikakati ya kiutendaji na hatua za kuendeleza elimu ya msingi.

Washikadau wengi wamekuwa wakihusishwa katika hatua mbalimbali za uundaji wa mpango huu. Vikundi kadhaa vya Kiufundi ambavyo vilihusisha wajumbe kutoka katika vikundi tofauti vya washikadau, ikiwa ni pamoja na mikutano ya kiushauri miongoni mwa sekta za wizara walichangia kwa kiasi kikubwa katika kuanzisha mfumo mzima wa mpango wa maendeleo ya elimu ya msingi.

Katika mpango huu wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi tunatambua kwamba utekelezaji wa sera muhimu na maelekezo ya kimkakati utahitaji kufanya kazi zaidi kwa kuendeleza mipango ya kina kuhusu aina ya programu, gharama, ugharamiaji, mipango ya utekelezaji, ratiba za utekelezaji, vitabu vya miongozo na maelekezo, uongozi, na taratibu za usimamizi na tathmini.

Ni makusudi yetu kuunganisha polepole miradi yote ya elimu inayoendelea na shughuli za programu katika Programu ya Mendeleo ya Sekta ya Elimu ili kupata uratibu mzuri wenye juhudi ya kuinua ubora wa elimu ya msingi, ikiwa ni pamoja na kuongeza upatikanaji wake na usawa.

Napenda kuwashukuru wale wote waliochangia katika utayarishaji wa Mpango huu wa Maendeleo.

Joseph J. Mungai (MB.)
WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI.

YALIYOMO **Ukurasa**

DIBAJI ii

YALIYOMO ii

VIFUPISHO iv

MUHTASARI WA UTENDAJI vi

1. UTANGULIZI 1

2. MAZINGIRA YA SERA 3

2.1. MSIMAMO WA TANZANIA KATIKA MALENGO YA ELIMU KIMATAIFA 3

2.2. SERA YA ELIMU NA MAFUNZO 3

2.3. PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA ELIMU 4

2.4 DIRA YA MAENDELEO TANZANIA 2025 5

2.5. MAKALA YA MKAKATI WA KUPUNGUZA UMASKINI 5

2.6. PROGRAMU UBORESHAJI SERIKALI ZA MITAA 6

3. MUUNDO WA MPANGO WA MAENDELEO 7

3.1. ONGEZEKO LA UANDIKISHAJI 7

3.1.1. Uandikikishaji na Fursa 8

3.1.2. Uajiri na Upangaji Walimu 9

3.1.3. Ujenzi 11

3.1.4. Watoto na vijana walio nje ya mfumo rasmi wa shule 13

3.2. KUINUA UBORA 15

3.2.1. Maendeleo ya Watumishi 15

3.2.2. Rasilimali za kufundishia na kujifunzia 17

3.3. KUJENGA UWEZO 18

3.3.1. Mafunzo ya Ualimu Tarajali 19

3.3.2. Utawala Bora 20

3.3.3. Usimamizi wa Fedha 22

3.3.4. Mfumo wa Habari wa Menejimentiywa Elimu 23

3.4 MIFUMO YA KITAASISI YA MPANGO WA MAENDELEO YA ELIMU YA MSINGI 24

3.4.1. Mipango ya Kiutawala 25

3.4.2. Majukumu ya Kitaasisi 26

Ngazi ya kijiji/Mtaa 26

Ngazi ya Kata 27

Ngazi ya Wilaya 28

Ngazi ya Mkoa 29

Wizara ya Elimu na Utamaduni 30

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa 32

Kamati ya Mendeleo ya Elimu ya Msingi 34

Kamati ya Uendeshaji ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu 35

Wahisani na Mashirika yanayotoa msaada 36

Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Jumuia za jamii 38

4. BAJETI 38

VIAMBATISHO vya kila kipengee cha:

1. Bajeti ya kawaida ya Elimu ya Msingi kwa kila kipengee 41

2. Muhtasari wa Gharama wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi 43

3. Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi 44

4. Uandikishaji katika Shule za Msingi 46

5. Mahitaji ya Mwalimu na Darasa 47

6. Gharama ya kila kipengee cha shule ya msingi 48

7. Gharama za Programu na matarajio kwa Watoto na Vijana walio nje ya mfumo rasmi wa shule. 49

8. Muundo wa Kitaasisi wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi. 51

ORODHA YA VIFUPISHO

BEDC	Kamati ya Mendeleo ya Elimu ya Msingi
CB	Kujenga Uwezo
CG	Ruzuku Maalum kwa kila mtoto
DED	Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya
EFA	Elimu kwa Wote
EMIS	Mfumo wa Usimamiaji wa Habari za Elimu
EPF	Mfuko wa Programu ya Elimu
ESDP	Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu
ETP	Sera ya Elimu na Mafunzo
GDP	Zao ghafi la ndani ya nchi
GER	Jumla ya kiasi cha Uandikishaji
D/S	Shifti Mbili
HIPC	Nchi Maskini zenye Madeni Makubwa
HT	Mwalimu Mkuu
IAE	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
IEC	Habari, Elimu na Mawasiliano
IFMS	Mfumo wa Usimamizi kamili wa fedha
DG	Ruzuku ya Maendeleo
INSET	Mafunzo ya Walimu Kazini
LGAs	Mamlaka ya Serikali za Mitaa
LGRP	Programu ya Kuboresha Serikali za Mitaa
M&E	Usimamizi na Tathmini
NECTA	Baraza la Mitihani la Taifa Tanzania
NFE	Elimu Isiyo Rasmi
NGO	Shirika lisilo la Kiserikali
MANTEP	Mafunzo ya Uongozi kwa Watumishi wa Elimu
MOEC	Wizara ya Elimu na Utamaduni
MOF	Wizara ya Fedha
MTEF	Mfumo wa Matumizi ya Kipindi cha Kati
PTR	Uwiano wa Mwalimu kwa Mwanafunzi
MMEM	Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi
PER	Mapitio ya Matumizi ya Umma
TAMISEMI	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PRSP	Makala kuhusu Mkakati wa Kupunguza Umaskini
PSRP	Programu ya Urekebishaji Huduma za Umma

RAS	Katibu Tawala Mkoa
RS	Sekretariati ya Mkoa
TAMISEMI	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TIE	Taasisi ya Elimu Tanzania
TLS	Hudumu za Maktaba Tanzania
UPE	Elimu ya Msingi kwa Wote
USD	Dola ya Kimarekani
UDSM	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
WEC	Mratibu wa Elimu Kata.

MUHTASARI WA UTENDAJI

Tanzania ni kati ya nchi zinazodumisha mikataba na makubaliano ya kimataifa inayohusu kuimarisha upatikanaji, usawa na ubora wa elimu. Tangu mwaka 1995 Serikali imeanzisha mfululizo wa sera na marekebisho katika sekta ya elimu kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba watoto WOTE wanapata fursa sawa ya elimu bora ya msingi. Hakuna mtoto atakayenyimwa fursa ya kupata elimu kwa sababu ya umaskini, jinsia, ulemavu, au kwa kukosa sare za shule, ada au michango yoyote ya wazazi, au kwa sababu ya kukosa nyenzo za kujifunzia, vifaa au walimu.

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ni Mpango wa miaka mitano unaoelezea dira ya Elimu ya Msingi kwa Wote ndani ya mfumo mpana wa sera ya Tanzania kuhusu sera ya Elimu na Mafunzo, na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu, Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa na Makala kuhusu Mkakati wa Upunguzaji Umaskini uliokithiri na Dira 2025. MMEM inajumuisha vipengele vikuu vinne: (a) Kuongeza idadi ya uandikishaji (b) Kuinua ubora wa michakato ya kufundisha na kujifunza (c) Kujenga uwezo ndani ya mfumo wa elimu na katika sekta nyingine za umma na utoaji wa huduma za elimu; na (d) Uimarishaji wa Mipango ya kitaasisi ambayo inasaidia upangaji na utoaji wa huduma za elimu.

Ili kufikia lengo la kuandikisha watoto wote wenye umri kati ya miaka 7 – 10 ifikapo mwaka 2005, MMEM inalenga katika masuala ya uandikishaji na upatikanaji, uandikishaji na usambazaji wa walimu na ukarabati na ujenzi wa madarasa. Pia inajumuisha mipango ya muda wa kati ya kupanua programu za elimu kwa watoto na vijana walio nje ya mfumo rasmi wa shule.

Lengo la kuinua ubora wa elimu litafikiwa kwa kuimarisha maeneo matatu. Kwa Watumishi, lengo la msingi ni katika kuendeleza taaluma ya walimu walio kazini, pamoja na juhudi za ziada zinazowalenga wakuu wa shule, kamati za shule na wakufunzi wa vyuo vya mafunzo. Kwa kupande wa rasilimali za kufundishia na kujifunzia, mkazo upo katika vitabu vya kiada na vifaa za kufundishia, ubora na umuhimu wa mtaala, na mazingira ya shule.

Kwa kuongezea katika pembejeo za mafunzo na vifaa vya kufundishia kama vilivyotajwa hapo juu, ubora wa elimu unategemea uwezo wa watu na mifumo. Kwa hali hiyo lengo la kujenga uwezo linazingatia juhudi katika kuanzisha utambuzi na mazoea ya kanuni za utawala na uongozi miongoni mwa washikadau wote wa elimu, hususan kamati za shule

na jumuiya. Hii inakamilisha juhudi za kuboresha ujuzi wa usimamizi wa fedha, kwa kulenga katika uwazi na uwajibikaji wakati wote katika mfumo. Mfumo ulioimarishwa wa usimamizi wa habari za elimu utatoa takwimu nyingi zinazohitajiwa na mameneja na wanamipango, na utakuwa utaratibu wa kufikia uwajibikaji wa kielimu. Mwisho, mafunzo kwa walimu tarajali yatatazamwa upya na kuimarishwa kwa lengo la kuongeza uwezo wake wa kutoa idadi kubwa ya walimu wapya wanaohitajika kuendana na ongezeko la uandikishaji, pamoja na kuimarisha ubora na umuhimu wa mafunzo ambayo walimu wanaoanza kazi watapatiwa.

Mwisho, chini ya kanuni za sekta pana ya maendeleo ya ushirikiano wa pamoja ambao unalinda utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi, uhusiano mpya wajibu na majukumu vimeelezwa kwa muhtasari.

1. UTANGULIZI

Tanzania imelenga kwa uangalifu mikakati yake ya maendeleo katika kupambana na ujinga, maradhi na umaskini. Uwekezaji katika mtaji wa watu unatambuliwa kama msingi katika kuinua ubora wa maisha ya Watanzania.

Tangu mwaka 1995, serikali imeanzisha mfululizo wa marekebisho katika elimu kupitia sekta pana ya programu ya maendeleo ili kushughulikia matatizo yaliyopo katika sekta. Changamoto zinazoikabili sekta ndogo ya elimu ya msingi zaidi ya yote zinatoka katika mfumo wa elimu ambao umekuwa ukijaribu kuelimisha idadi kubwa ya watoto kutoka katika kaya zilizo maskini kiasi. Wakati wote huo, jambo hili limekuwa likifanyika kwa kujibana kutokana na upungufu mkubwa wa rasilimali ya umma. Kushughulikia masuala haya si zoezi lililo wazi kwa sababu matatizo na chanzo chake vinaingiliana, vyote kwa pamoja ndani ya mfumo wa elimu wenyewe, na kutokana na mambo mengi yaliyo nje ya sekta ya elimu.

Ndani ya mfumo wa elimu matatizo makubwa zaidi yanahusishwa na mkusanyiko wa vipengee ambavyo vinaunga mkono ubora wa jinsi ya kufundisha na kujifunza darasani. Watoto wengi wanasoma wakiwa wamesongamana, kwenye vyumba vya madarasa visivyo na samani na ambavyo havijamalizika kujengwa na mara kwa mara imewalazimu kushirikiana vitabu vichache vya kiada walivyokuwa navyo. Walimu walio wengi hawana ujuzi wa kutosha na utaratibu usioridhisha wa upangaji walimu, lakini kwa hali yoyote ile mara nyingi wanajaribu kufanya kazi nzuri kwa kutumia rasilimali chache za msingi. Aghalabu mtaala unaonekana kuwa mpana sana na kwa upande fulani hauna manufaa kwa wanafunzi walio wengi na kwa mahitaji yao kimaisha. Walimu walio wengi, wakuu wa shule na wafanyakazi wengine katika elimu hawakuandaliwa vizuri kwa ajili ya uongozi na kazi bora ya kujiamini wanayohitajiwa kufanya kama wajibu wao; lakini mara nyingi anajitahidi kufanya kazi kadri ya uwezo wao katika mazingira yenye upekee na yenye rasilimali duni.

Kipengele muhimu kutoka nje ambacho sekta ya elimu inapaswa kukishughulikia ni shinikizo kubwa la uchumi wa umma na binafsi ambalo limesababisha maendeleo ya kiuchumi kwenda taratibu. Kaya nyingi zenye rasilimali chache kifedha zinapata taabu katika kuamua kuhusu kuwekeza katika elimu ya watoto wao. Kwa miaka mingi uandikishaji wa watoto na kiwango cha mafanikio

kimekuwa kikishuka, wakati ambapo utoro na kuacha shule vinaongezeka. Hivi sasa athari za kutisha za maambukizo ya virusi vya UKIMWI na migogoro ya kijamii zimekuwa na matokeo mabaya katika uwezo wa binadamu kuendesha mfumo wa elimu, pia katika mitazamo ya kielimu kwa watoto walioathirika kwa UKIMWI. Hatimaye, changamoto muhimu kutoka nje inaongezeka kwa hamu ya Tanzania kutaka kuchukua nafasi katika uwanja mpya kiulimwengu kwa mahitaji yanayofuatana ya mtu binafsi na ya taifa yanayolenga katika maendeleo mapya kiteknolojia.

Mpango huu wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ni moja kati ya matokeo ya kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) na yatahusisha utoaji elimu ya msingi ikiwa ni pamoja na elimu kwa watoto na vijana walio nje ya mfumo rasmi wa shule. Malengo ya umuhimu wa uwekezaji ni: Kuongeza idadi ya uandikishaji unaolenga katika ujenzi wa madarasa, kuajiri walimu, na upangaji wa walimu; kuinua ubora, kunakojumuisha mafunzo ya walimu walio kazini na tarajali, na utoaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia; na kuimarisha mfumo mpana wa kuinua uwezo wa utawala kupitia katika juhudi maridhawa za kujenga uwezo. Waraka huu unaonyesha mfumo wa mpango mzima; Mipango ya utekelezaji na bajeti kwa kina vinapatikana katika nyaraka zilizoambatishwa.

Katika shule za msingi za Tanzania kuna watoto 4,842,875. Hata hivyo, inakadiriwa kwamba ifikapo mwishoni mwa Januari 2002 kutakuwa na watoto milioni tatu wenye miaka 7 – 13 ambao watakuwa hawajaandikishwa shule. Kama wote watapata nafasi kwa wakati mmoja,

jumla ya uandikishaji wa watoto katika shule za msingi Januari 2002 itaongezeka kwa theluthi moja kutoka takriban watoto milioni 4.8 mpaka milioni 7.5. Kwa kuwa uandikishaji huu utazidi rasilimali za mfumo wa elimu, MMEM inachukua hatua za uandikishaji za taratibu ili kuweza kufanikisha taratibu Elimu ya Msingi kwa Wote (UPE).

2. MAZINGIRA YA SERA

2.1. MSIMAMO WA TANZANIA KATIKA MALENGO YA ELIMU

Mkutano wa Dunia wa Jomtien kuhusu Elimu kwa Wote (EFA) wa mwaka 1990 ulikuwa njia ya kutambua malengo yaliyokubaliwa kimataifa katika utoaji wa elimu kama haki ya msingi ya binadamu. Tanzania pia ni sehemu ya mfumo wa utekelezaji wa Dakar 2000, mapitio ya kimataifa

ya maendeleo ya elimu tangu Jomtien, na imeungana na mataifa mengi ambayo yameridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto.

Hata hivyo, ni kampeni ya Elimu ya Msingi kwa Wote ambayo inabakia kuwa msingi wa maazimio ya Tanzania kutimiza matakwa ya EFA. Kanuni zake za fursa, usawa na ubora kwa watoto wote zinategemea nyingi kati ya sera zilizoingizwa katika mpango huu wa maendeleo ya elimu ya msingi.

2.2. SERA YA ELIMU NA MAFUNZO

Hamu ya Serikali kuimarisha utoaji na ubora wa elimu imesababisha kuundwa kwa Sera ya Elimu na Mafunzo (ETP) ya mwaka 1995. Sera ya Elimu na Mafunzo (ETP) inajumuisha sekta nzima ya elimu na mafunzo. Malengo makuu ya sera hii ni kuongeza idadi ya wanaoandikishwa, fursa sawa, kuinua ubora, upanuzi na matumizi yanayofaa ya nyenzo na utendaji wenye ufanisi katika mfumo mzima.

Sera nyingine pana zaidi inajumuisha kuongeza ubia katika utoaji elimu, kupanua msingi wa kifedha na gharama za elimu zinazofaa na kurahisisha miundo ya menejimenti ya elimu kwa kukabidhi madaraka katika shule, jumuia na mamlaka ya serikali za Mitaa (LGAs).

2.3. PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA ELIMU

Kufuatia ETP, mtazamo mpana wa sekta kuhusu maendeleo ya elimu ulibuniwa ili kusaidia kukamilisha mpango wa muda mrefu wa serikali wa maendeleo ya watu na shabaha ya kukomesha umasikini, na kurekebisha tatizo la uvamizi usiyokwisha. Umuhimu wa mkabala mpana wa sekta uliochukuliwa katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) ni ushirikiano wa washikadau, kwa kuweko umoja wa watu, fedha na rasilimali bidhaa kwa shughuli za mipango, utekelezaji, usimamizi na tathmini ya elimu. Mkabala huu unaanzisha uhusiano mpya ambao unakuza ubia, uratibu na umiliki miongoni mwa makundi yote ya watu walio na shauku katika elimu

Programu ya Maendeleo ta Sekta ya Elimu ni shughuli pana ambayo imechukua malengo yake kutoka Sera ya Elimu na Mafunzo. Malengo

ambayo yana manufaa kwa sekta ndogo ya elimu ya msingi yanajumuisha: juhudi mbalimbali kuinua ubora wa utoaji wa elimu, kuongeza na kuboresha katika fursa na usawa kwa watoto wote, utoaji madaraka katika miundo ya utawala, kukabidhi madaraka katika kiwango cha jamii, na kupanua msingi wa kifedha unaosaidia mfumo wa elimu.

Mpango huu kwa elimu ya msingi umechukuliwa katika mipango mikuu ya elimu ya msingi na elimu ya ualimu. Mipango mikuu kwa elimu ya sekondari na elimu ya juu iko katika hatua ya kuendelezwa.

2.4. DIRA YA MAENDELEO TANZANIA 2025

Dira ya Maendeleo Tanzania ya 2025 inafikiria kuutokomeza kabisa umaskini ifikapo mwaka 2025 na hivyo kufikia kipaumbele kikubwa katika sekta ya elimu ambayo inachukuliwa kama msingi katika kuleta

mabadiliko kijamii na kiuchumi. Inaelezwa kwa dhati katika waraka wa Dira ya 2025 kwamba:

"Elimu ichukuliwe kama nguvu za asili za kimkakati kwa kuweka mageuzi ya akili na kwa kuunda taifa lililoelimika vizuri, lenye maarifa ya kutosha yanayohitajika katika kutatua kwa ufanisi na kiushindani changamoto ya maendeleo inayoikabili nchi. Kutokana na hilo, mfumo wa elimu hauna budi kupangwa upya na kubadilishwa kwa ubora unaolenga katika kukuza ubunifu na utatuzi wa matatizo" (uk.10)

Dira ya 2025 ni uundaji wa taifa lililoelimika vizuri na maisha bora kwa watanzania wote. Mpango huu wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ni mpango unaoanzishwa kwa ajili ya kufikia shabaha za elimu zilizoelezwa katika Dira.

2.5. MAKALA KUHUSU MKAKATI WA KUPUNGUZA UMASKINI

Makala kuhusu Mkakati wa kupunguza Umasikini (PRSP) ni mkakati wa muda wa kati uliowekwa katika muktadha nafuu wa deni wa Nchi Maskini Zenye Madeni Makubwa (HIPC) na kuendelezwa kupitia mashauriano ya viwango mbalimbali katika: (i) Kupunguza umasikini

wa kipato (ii) Kuimarisha uwezo wa watu, kuishi na hali ya maisha; na (iii) Kujumuisha madhara makubwa miongoni mwa masikini.

Elimu inawawezesha watu kutumia uwezo wao na kuongeza nguvu katika kipato. Pia inampa mamlaka mtu mmojammoja kushiriki katika mabadiliko ya maisha yake na ya jamii kwa ujumla. Ukosefu wa elimu ya msingi unadhoofisha juhudi za kuboresha afya na lishe, kupunguza vifo vya watoto wachanga, mama wakubwa na kushughulikia chanzo na athari za virusi vya UKIMWI. Kwa kuzingatia uwezo mkubwa

wa taifa lililoelimika vizuri katika kustawi kiuchumi na kijamii, kupatikana kwa elimu ya msingi kwa wote (UPE) ni lengo la Maendeleo la kupewa kipaumbele. Makala ya kuhusu Mkakati wa Kupunguza Umaskini (PRSP) inasisitiza tena kwamba elimu ipo katika kiini cha maendeleo na imeyapa kipaumbele maendeleo ya sekta ya elimu katika juhudi za kupunguza umaskini. PRSP inatoa utaratibu wa kutamka sera ya Serikali ya maendeleo ya jumla. Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu na mipango yoyote ya sekta ndogo inafanya kazi ndani ya muundo huu muhimu. Pia PRSP inatoa utaratibu ambapo inatazama na kuelekeza usaidizi na misaada ya kimataifa dhidi ya vipaumbele vya maendeleo vya serikali yenyewe.

2.6. PROGRAMU YA UBORESHAJI WA SERIKALI ZA MITAA

Programu ya sasa ya kurekebisha Huduma za Umma inalenga katika kuboresha utendaji katika utoaji wa bidhaa na huduma. Programu ya Uboreshaji serikali za Mitaa (LGRP) ni sehemu muhimu ya marekebisho makubwa ya sekta ya umma. Ni utaratibu wa awali katika kutoa na kukabidhi madaraka katika kiwango cha jamii, sifa kuu katika kutoa elimu kwa kiwango cha msingi. MMEM imewekwa imara ndani ya mfumo wa kutoa madaraka na inajumuisha vipengele ambavyo vitasaidia kuinua uwezo wa watumishi na miundo katika kiwango cha jamii, kuwawezesha kushiriki katika mipango mikubwa na utoaji wa huduma bora za elimu ya msingi.

3. MUUNDO WA MPANGO WA MAENDELEO

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi una vipaumbele mkakati vinne: Ongezeko la uandikishaji, kuinua kiwango cha ubora, kujenga uwezo, na

matumizi ya hali ya juu ya rasilimali za watumishi, vifaa na fedha. Sehemu nne za MMEM zimejengwa katika vipaumbele mkakati hivi. Sehemu hii inaeleza kwa muhtasari kila kipengele kikuu, na tena kueleza kwa undani kila kipengele kidogo pamoja na malengo na mikakati.

Hivi sasa kuna miradi ya elimu inayoendelea ambayo inashughulikia vipengele vya kuboresha elimu ya msingi. Miradi yote hiyo inachangia katika maendeleo ya elimu na kwa kupitia shughuli zake mbalimbali inatoa utambuzi katika uhalisi wa utoaji wa elimu. Shughuli hizi za mradi zitaingizwa polepole katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi.

3.1 ONGEZEKO LA UANDIKISHAJI

Umuhimu mkubwa katika elimu ya msingi ni kuongeza uandikishaji wa jumla yote na halisi ya wasichana na wavulana. Uongezaji huu utafanywa kwa kuzingatia mchanganyiko wa mikakati: (a) Kuongeza viwango vya uandikishaji wa makundi yote ya watoto; (b) Kuwatumia ipasavyo walimu na madarasa yaliyopo; (c) Kuandikisha walimu wapya na kujenga madarasa mapya; na (d) Kupanua programu ya elimu kamilishi kwa watoto na vijana walio nje ya mfumo rasmi wa shule. Vipengele vidogo vinne vimeundwa kutoka katika mikakati hii

3.1.1 Uandikishaji na Fursa

Malengo ya uandikishaji yaliyoingizwa katika mpango huu yataleta maendeleo ya haraka katika kupatikana kwa UPE, lakini yamejikita katika kukua kwa mikakati inayowezekana ambayo inaangalia makadirio halisi ya watu, vifaa na rasilimali za fedha.

Serikali inakusudia kuongeza uandikishaji kuanzia milioni 1.5 katika mwaka 2002 na kuendelea mpaka mwaka 2006. Kipaumbele cha uandikishaji kitatolewa kwa watoto wenye umri wa miaka saba. Hata hivyo, kamati ya shule itaamua kama iandikishe watoto wakubwa kutegemeana na hali inavyoruhusu.

Serikali imeanzisha Mfuko Maalum wa Elimu ya Taifa kulipia elimu ya watoto kutoka kwenye makundi yenye matatizo wakiwemo yatima walioathirika na UKIMWI. Kwa utaratibu huu inakusudiwa kuwa wasichana na wavulana wote wanaweza kuandikishwa shule.

MALENGO

1. Kuwaandikisha darasa la kwanza watoto wote wenye umri wa miaka 7-12 ifikapo mwaka 2005:

Lengo la Maingizo Mapya:	2002:	1,500,000
	2003:	1,600,000
	2004:	1.640,969
	2005:	1,041,880
	2006:	1,065,843

2. Kuhakikisha kwamba mfumo wa elimu rasmi unaweza kutoa nafasi kwa idadi kubwa ya watoto wenye umri wa kwenda shule.
3. Kuhakikisha wasichana wote na wavulana kutoka katika makundi ya wenye matatizo ikiwa ni pamoja na yatima walioathirika na UKIMWI wanaandikishwa.

MIKAKATI

1. Serikali itafuta ada za shule na michango yote ya lazima inayotolewa na wazazi kuanzia Julai 2001 ili pasiwepo mtoto yeyote atakayenyimwa haki ya kusoma.
2. Serikali itaanzisha msaada wa masomo kutoka katika Mfuko wa Elimu wa Taifa kwa ajili ya kuwalipia elimu watoto wenye matatizo, ikiwa ni pamoja na yatima walioathirika na UKIMWI.
3. Habari ya vyombo mbalimbali vya habari, Elimu na Mawasiliano (IEC) zitafanywa kuwahamasisha wazazi, viongozi wa mtaa na kijiji, washauri na watumishi wa mamlaka za serikali za Mitaa katika viwango vyote kuhusu MMEM na vidokezo vyake.
4. Kipimo cha uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi ni 1:45.
5. Uwezo wa shule kwa kuzingatia upangaji wa walimu na nafasi darasani utahakikishwa kwa kuongeza utumiaji wa walimu na madarasa kwa shifti mbili na ufundishaji wa madaraja mbalimbali, kama hatua ya kiasi na ya muda.

Mkakati wa jumla wa kufikia uandikishaji kamili ifikapo 2004:

2002: Kuingiza watoto wote wenye umri wa miaka 7 na ikiwezekana wenye miaka 8.

2003: Kuingiza watoto wote wa mwaka 2003 wenye miaka 7, wote wenye miaka 8 waliobakia 2002, na waliobaki 2002 wenye miaka 9 (ambao sasa wana miaka 9 na 10).

2004: Kuingiza watoto wote wa mwaka 2004 wenye miaka 7 na wale wote waliobaki 2002 wenye miaka 9-10 (ambao sasa wana miaka 11-12).

2005 na 2006: Kuingiza watoto wote wenye umri wa miaka 7

3.1.2 Uajiri na Upangaji Walimu

Serikali itazisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandikisha, kufundisha na kupanga idadi ya kutosha ya walimu wa shule za msingi kwa namna ambazo zitafaa kukabiliana na ongezeko kubwa la uandikishaji wa watoto, na kuongezeka kwa kiwango cha matatizo ya wafanyakazi yanayosababishwa na mambo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na vifo vinavyosababishwa na ugonjwa wa UKIMWI.

MALENGO

1. Kuandikisha idadi ya kutosha ya walimu wapya

Malengo ya kuajiri walimu wapya:	2002:	9,047
	2003:	11,651
	2004:	10,563
	2005:	7,286
	2006:	7,249

2. Kuanzisha uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi ambao utasaidia ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa.
3. Kuhakikisha kunakuwepo na mgawanyo sawa na wenye uwiano wa kijinsia wa walimu waliopata mafunzo.
4. Kuongeza muda wa mwalimu na mwanafunzi kukutana kupitia usimamizi unaofaa wa mwalimu.

[1]MIKAKATI

1. Kampeni za utangazaji zitalenga walimu wenye ujuzi wa hali ya juu, zikitilia mkazo matarajio ya kazi nzuri na masharti ya utumishi. Juhudi zitafanywa kupunguza au kuondoa vikwazo vya kifedha vinavyowakumba walimu wapya.
2. Upangaji upya wa vivutio, ajira na kuandikisha walimu wapya vitafanywa.
3. Kipimo cha uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi ni 1:45.
4. Kivitendo, baadhi ya shule zitahitaji kuwa na vipindi vya asubuhi na vipindi vya mchana kwa miaka kadhaa. Inakusudiwa kwamba asilimia 11 ya walimu watafundisha shifti mbili mwaka 2002, asilimia 18 mwaka 2003, na asilimia 25 kuanzia mwaka 2004 mpaka 2006[1]. Pia itakuwa ni muhimu kwa baadhi ya walimu kufundisha wanafunzi wa madaraja tofauti katika darasa moja kwa muda uliopangwa.
5. Maelekezo na kujenga uwezo vitatolewa kwa walimu na walimu wakuu kuhakikisha kwamba ufundishaji wa kutumia darasa moja kwa madaraja mengi na shifti mbili unaanza kutekelezwa.
6. Muda wa chini wa ufundishaji kwa wiki shuleni utakuwa ni saa 20 za kufundisha.
7. Patakuwa na uhakika wa maendeleo ya kutosha ya walimu wanaoanza kazi na walio kazini.

3.1.3 Ujenzi

Serikali itaanzisha programu ya ujenzi wa darasa ambayo itatoa madarasa ya kutosha na nyenzo za usafi kwa ajili ya ongezeko la uandikishaji.

Mchanganyiko wa vielelezo vinavyofaa kwa ujenzi wa darasa utachukuliwa ambao utazingatia hali halisi ya jumuia. Utaratibu mkuu wa utoaji fedha wa MMEM ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa na kamati za shule zinaweza kuanzisha programu ya ujenzi utakuwa wa Ruzuku ya Maendeleo (DG). Serikali imeanzisha Ruzuku ya Maendeleo (DG) kwa lengo la jumla la kuinua ubora wa miundo mbinu katika shule za msingi. Itafanya kazi katika

mazingira ya kugawa madaraka na kufuata mahitaji katika wilaya.

Pia, nyumba za walimu zitajengwa, hasa maeneo ya vijijini na yaliyo mbali.

MALENGO

1. Kufanya matengenezo ya madarasa yaliyopo kwa asilimia 2-3 kwa mwaka.
2. Kujenga madarasa mapya ya nyongeza, hasa katika miaka mitatu ya mwanzo wa mpango ili kuendana na ongozeko la uandikishaji wa watoto wenye miaka 7-10 linalotarajiwa.

Malengo ya ujenzi wa madarasa mapya:	2001:	13,868
	2002:	13,396
	2003:	14,203
	2004:	6,794
	2005:	5,832

3. Kutoa nyumba za walimu kama kivutio cha upangaji kwa kutoa kipaumbele kwa walimu wa kike katika maeneo yaliyo mbali sana na yale ya vijijini.
4. Kutoa nyumba kwa walimu wapya kwa asilimia 30 kwa mwaka.

MIKAKATI

1. Asilimia 67 ya madarasa yatatumika kwa msingi wa shifti mbili kuanzia mwaka 2002 mpaka 2006.
2. Uamuzi kuhusu vipaumbele vya ujenzi wa darasa utazingatia Ruzuku ya Maendeleo na uhaba wa madarasa katika ratiba ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs).
3. Kamati za shule zitachukua jukumu la ujenzi. Zitakuwa na uwezo wa kuchagua kutoka katika michoro yenye viwango tofauti yenye gharama ya Dola za Kimarekani 4,000 kwa kila darasa. Shule zinaweza pia kuomba fedha kutoka kwenye Ruzuku ya Maendeleo (DG) ili kutosheleza gharama za vifaa vya usafi au nyumba za walimu. Fedha za Ruzuku ya Maendeleo (DG) zilizoidhinishwa zitatolewa katika akaunti ya benki ya shule

[1] Ingawa idadi ni kubwa katika kipindi cha MMEM, asilimia hizi zitaanza kupungua muda mfupi baada ya kipindi cha MMEM wakati ambapo uandikishaji unapungua, wakati huohuo walimu wapya na madarasa wanatumika katika mfumo.

kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo Baraza litahusika kikamilifu. Kwa hali hiyo Mkurugenzi wa Baraza anabaki kuwajibika katika matumizi mazuri ya Ruzuku ya Maendeleo (DG) wakati Kamati ya shule itawajibika kwa Baraza la Kijiji na kwa Mkurugenzi wa Baraza. Jumuia zitakuwa na uwezo wa kuunganisha fedha zao, watumishi au rasilimali nyingine na Ruzuku ya Maendeleo (DG) kuimarisha viwango vya michoro. Wahandisi wa wilaya watatoa msaada wa kiufundi.

4. Mgawanyo wa fedha kwa ujenzi wa nyumba za walimu utatoa kipaumbele katika maeneo ya vijijini na yaliyo mbali. Vigezo vya ugawaji vya DG kwa vitazingatia kwa kufuata msingi wa mahitaji ya ujenzi wa nyumba katika mpango wa elimu wa mwaka wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

3.1.4 Watoto na Vijana walio nje ya mfumo rasmi wa shule

Inakadiriwa kwamba zaidi ya watoto na vijana wa Tanzania milioni tatu wenye umri kati ya miaka 7 na 8 wameacha shule au hawajawahi kuandikishwa. Idadi hii kubwa inaweza ikapungua kwa kufuta michango ya lazima iliyopangwa kuanza Julai 2001, wakati ambapo ongezeko la watoto milioni 1 mpaka 1.5 wanategemea kuandikishwa. Hata hivyo, tukichukulia uwezo wa mfumo wa elimu rasmi na rasilimali finyu zinaelekea kuwemo katika elimu kwa maisha yanayotabirika ya baadaye, inawezekana kwamba idadi kubwa ya wasichana na wavulana kutoka katika umri uliotajwa inaelekea kubakia nje ya mfumo rasmi.

Mikabala ya elimu isiyo rasmi itapanuliwa kwa kupitia jitihada mbalimbali na kwa watoaji kwa lengo la kushughulikia limbikizo la vijana ambao hawajasoma Tanzania. Ongozeko hili litasaidiwa na kampeni ya Habari, Elimu na Mawasiliano (IEC) ambayo (a) itatilia mkazo umuhimu wa elimu kwa maisha ya baadaye ya mtu binafsi na jamii. (b) kuwahamasisha watu kujiandikisha katika programu za elimu na, (c) kupunguza kwa kiasi kikubwa uwezekano wa mtu yeyote kuacha shule. Kanuni zinazolinda jitihada hizi za elimu zitakuwa kwamba kila juhudi itakuwa kuwaingiza watoto katika mwelekeo na utoaji rasmi. Hii ina

maana mikakati ya programu kamili ya elimu imebuniwa kwa kipindi cha muda mfupi na wakati tu.

MALENGO

1. Kupanua programu za ziada za elimu ya msingi kwa watoto walioachwa katika mfumo rasmi, wakiwemo yatima wa waathirika wa UKIMWI.

MIKAKATI

1. Upeo uliopo wa programu ya elimu isiyo rasmi utapanuliwa kujumuisha vituo 11,325[2] ifikapo mwaka 2006 vitakavyowapatia elimu wanafunzi 906,000.
2. Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika yasiyo ya kiserikali NGOs na jumuia zitashiriki kwa kufungua vituo maalumu au kwa kutumia nyenzo zilizopo za shule ili kusaidia programu kama hizo za elimu iliyo nje ya mfumo rasmi wa shule.
3. Mikabala ya elimu iliyo nje ya mfumo rasmi itaingizwa katika mfumo wa shule ulio rasmi kama unafaa.

4. Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi kwa kushirikiana na Kamati ya Mafunzo ya Ufundi na Maendeleo zitaunda Sera ya Taifa inayoweza kubadilika kulingana na mikakati ya kushughulika na vijana walio nje ya mfumo rasmi wa shule, wakati zikiendelea kuhimiza maendeleo ya uandikishaji mzima wa wasichana na wavulana katika sekta ya elimu.[1]

3.2 KUINUA UBORA WA ELIMU

Umuhimu wa pili wa sera ya elimu ya msingi ni kutoa upya matumaini na kuboresha elimu ya shule za msingi, kwa kulenga katika sehemu kuu tatu: (a) Kuboresha mitindo na mbinu za ufundishaji wa walimu darasani; (b) Kuhakikisha upatikanaji wa vifaa bora vya kufundishia na kujifunzia; na (c) Kuhakikisha kuna msaada unaotakiwa ili kudumisha viwango vya elimu. Lengo ni kuboresha mafanikio yote ya watoto wa kike na wa kiume katika mfumo wa elimu ya msingi.

[1] Kituo" ni shule yoyote ya msingi au jengo lolote la umma lililochaguliwa na jumuia kutumika kwa shughuli za NFE

3.2.1 Maendeleo ya Watumishi

Mwalimu darasani ni chombo muhimu katika kuleta mafanikio bora katika kujifunza. Ubora kama huo unafikiwa kama kuna uwezekano na mazingira yanayochochea hali hiyo, ambapo wanaojifunza wanashiriki kikamilifu katika kujifunza, na pale ambapo wanafunzi, walimu na shule wanayo fursa ya kukua kibinafsi na kitaasisi.

Katika kipindi cha programu ya MMEM uboreshaji wa taaluma ya walimu utaendelea. Hata hivyo, mkazo katika mafunzo mengi utakuwa ni katika kuendeleza taaluma ya walimu, wakufunzi, wakaguzi na viongozi wengine wa elimu.

MALENGO

1. Kuwawezesha walimu kupata na kuendeleza ujuzi unaofaa wa ufundishaji ambao ni wa kitaaluma, upendo kwa watoto na kujali jinsia.

2. Kuwawezesha walimu kupata sifa za juu kitaaluma.

3. Kuwawezesha wafanyakazi wanaosaidia katika elimu, ambao ni wakaguzi, Waratibu Elimu Kata, wakufunzi na Walimu Wakuu, kutoa msaada unaotakiwa kwa walimu.

MIKAKATI

1. Programu kadhaa zisizo na gharama za mafunzo kazini ambazo hazitachukua idadi kubwa ya walimu shuleni zitaanzishwa.
2. Maudhui ya programu ya mafunzo ya walimu wanaoanza kazi na walio kazini itawaelimisha walimu na kuwapa fursa ya kupata na kuendeleza ujuzi unaofaa wa ufundishaji ambao ni wa kitaaluma urafiki kwa mtoto, na kujali jinsia, ikiwa ni pamoja na ujuzi wa mtu binafsi ambao unazingatia tatizo la sasa la virusi vya UKIMWI.
3. Muungano na mtandao wa mafunzo ya wanaoanza kazi na walio kazini kupitia programu inayofika mbali utaanzishwa na kuimarishwa.

4. Vituo zaidi vya mafunzo vvyae shule vitaanzishwa.
5. Shilingi 33,200 (Dola za Kimarekani 40) zitatolewa kwa mwalimu kwa siku kumi za mafunzo kazini kwa kila mwalimu kwa mwaka.
6. Kutoa fursa ya kujiendeleza kitaaluma kwa Wakufunzi, Wakaguzi, Walimu Wakuu, Waratibu wa Elimu Kata, Wasimamizi na Viongozi wengine wa Elimu.

3.2.2 Rasilimali za Kufundishia na Kujifunzia

Michakato ya ubora wa elimu itahimizwa kwa upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyohusika. Vitabu vya kiada ni kigezo kimojawapo muhimu katika mafanikio ya kujifunza na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi imekifanya kuwa sehemu muhimu ya kutiliwa mkazo. Kigezo kingine muhimu ni uhusiano wa mtaala kwa mazingira na changamoto ya maisha inayowakabili watoto wa Tanzania kwa sasa na hapo baadaye.

Wakati shule inapokuwa na ustadi zaidi katika kutoa Mpango wake Mzima wa Maendeleo ya Shule, Ruzuku ya MMEM kwa kila mtoto itakuwa ni utaratibu muhimu katika kupata vitabu vya kiada na vifaa vingine ambavyo vitachochea michakato mizima ya kujifunza na kufundisha, na kutoa vipengee visivyo vya mshahara ambavyo vitaboresha mazingira ya jumla ya kujifunza. Ruzuku ya Maendeleo kwa pamoja na pembejeo katika jumuia vitatolewa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa madarasa na vifaa vya usafi.

MALENGO

1. Kutumia utaratibu wa mahitaji ya kutoa madaraka na kusambaza ili kutoa vifaa bora vya kutosha na vya mafunzo kwa idadi ya watoto wote walio shuleni.

Malengo ya Utoaji[3] wa kitabu vya kiada:

2002: Uwiano wa Wanafunzi 3 kwa kitabu kimoja (3:1).

2006: Uwiano wa Mwanafunzi 1 kwa kitabu 1 (1:1). 2002:

2. Kutoa vifaa vya kutosha vya mafunzo ili kusaidia mahitaji ya mtaala.
3. Kuunda mazingira ya madarasa na ya shule yanayofaa kwa kujifunzia.

MIKAKATI

1. Ili kuanzisha mkondo wa fedha wa kutumainiwa katika kiwango cha shule kwa gharama zilizo nje ya mshahara, Ruzuku iliyo sawa na dola za Kimarekani 10 kwa kila mtoto anayeandikishwa itaanzishwa kitaifa ifikapo Januari 2001. Kati ya hizo, dola 4 kwanza zitapelekwa wilayani ili kuziwezesha shule kupata vitabu vya kiada na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia. Dola 6 zinazobakia zitatolewa katika shule kupitia baraza la wilaya na kamati za shule zitaamua njia bora za kutumia fedha hizo.

Kamati za shule zitaendeleza ubia na sekta za umma/binafsi katika ngazi ya Jumuia, wakati ambapo ubia kama huo katika ngazi za wilaya na kitaifa pia zitaendelezwa kwa nia ya kuwekeza katika vifaa vya shule.

2. Mfumo uliopo wa kutoa madaraka ya utafutaji wa vitabu vya kiada utaanzishwa na kuenezwa kwa Mamlaka zote za serikali za mitaa na katika ngazi ya shule.

3. Shule zitatumia Mpango Mzima wa Maendeleo ya Shule kuchagua vifaa vya kufundishia.

3.3. KUJENGA UWEZO

Mkakati wa tatu wa sera ya elimu ya msingi ni kuimarisha uwezo wa taasisi na ustadi wa ngazi za kati, Mamlaka za Serikali za Mitaa na za shule. Mkakati huu unaendana na sera za Serikali za kupata ufanisi mkubwa, uundaji upya wa utumishi na serikali za mitaa, kugawa madaraka ya shughuli za serikali na kuingiza kanuni za ushirikishwaji na uwezeshaji kwenye huduma ya umma.

[3] Wastani wa gharama ya kitabu kimoja ni (Dola za Kimarekani 4)

3.3.1 Mafunzo ya Walimu tarajali

Idadi kubwa ya walimu watapata mafunzo katika kipindi cha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi kuwapatia sifa zinazofaa na ujuzi wa ufundishaji. Ili kufanikisha jambo hili mtaala, muda na mpangilio wa kozi za mafunzo ya ualimu na nyenzo katika vyuo vya mafunzo ya ualimu vitapitiwa kwa pamoja sambamba na lengo hili. Kwa kuongezea, programu ya kuboresha sifa za wakufunzi itaanzishwa.

MALENGO

1. Kuboresha sifa, maarifa na ujuzi wa wakufunzi wa vyuo vya ualimu.
2. Kuhakikisha kwamba walimu wapya wana ujuzi wa kufundisha na maarifa yanayofaa.
3. Kutambua kiwango na utoaji wa mafunzo ya walimu wanaoanza kazi ili kufanikisha matumizi ya raslimali za watu, fedha na vifaa katika mfumo wa mafunzo ya ualimu.
4. Kutoa mafunzo kwa idadi inayotakiwa ya walimu wa daraja A.

MIKAKATI

1. Kampeni za kutangaza zitawalenga wanafunzi wa ualimu wenye uwezo wa hali ya juu, zikitilia mkazo matarajio mazuri ya kazi na masharti ya utumishi. Juhudi zitafanywa kupunguza au kuondoa vikwazo vya kifedha vinavyowakumba walimu wapya.

2. Mtaala wa mafunzo utapitiwa upya ili kusisitiza uendelezaji wa maarifa ya, na uwezo wa ufundishaji na usimamizi kiwango cha darasani.
3. Idadi ya wanafunzi wapya wa ualimu itafikia 9,000 mwaka 2002, 10,000 kwa kila mwaka kwa miaka ya 2003-2005, na 9,000 mwaka 2006.
4. Wakufunzi waliopo watapitia katika programu ya kuboresha ujuzi na maarifa na wakufunzi wapya wataajiriwa.
5. Mfumo wa mpangilio, muda na operesheni nzima ya mafunzo ya walimu wanaoanza kazi utapitiwa upya na kuongezwa ufanisi.
6. Uwezo wa usimamizi, na rasilimali za vifaa na fedha za vyuo vya ualimu utaimarishwa.

7. Ratiba ya mafunzo ya wakufunzi itapitiwa upya kuhakikisha kwamba wanaweza kupangwa katika shule ili kukagua mazoezi ya kufundisha, na kwa ajili ya kuendesha mafunzo kazini.

3.3.2 Utawala Bora

Mafunzo ya uongozi yatatolewa kwa wakuu wa shule, kamati za shule, wasimamizi wa elimu kata, wakaguzi, na kwa wafanyakazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mkoa na Taifa. Mkazo utakuwa katika kupata ujuzi katika mipango yote ya maendeleo ya shule, mipango ya wilaya ya maendeleo ya elimu na mipango ya elimu ya taifa. Masuala ambayo mipango yote itazingatia ni pamoja na athari za virusi vya UKIMWI katika mfumo wa elimu, kuhakikisha usawa wa jinsia na udhibiti. Lengo zima ni kuboresha uongozi, wajibu na ufanisi kipindi chote cha mfumo ili watoto wapate elimu bora.

MALENGO

1. Kuanzisha au kuimarisha stadi za uongozi wa elimu.

2. Kupanua katika shule zote dhana na ustadi wa Mipango kamili ya Maendeleo ya shule
4. Kuhakikisha kwamba kamati za shule zina uwiano wa kijinsia, zinaundwa kidemokrasia na zinajumuisha washikadau wakuu wote.

MIKAKATI

1. Wafanyakazi na washikadau wote wanaowajibika moja kwa moja na utekelezaji wa MMEM watapewa taarifa na miongozo ya msingi ya MMEM
2. Masuala ya virusi vya UKIMWI, jinsia na udhibiti yataelekezwa katika mafunzo yote ya uongozi.
3. Zoezi lililopo la upangaji wa shule litaendelea likihusisha wilaya zote.
4. Wafanyakazi na washikadau wote wanaowajibika moja kwa moja na uongozi wa MMEM watapewa mafunzo kuhakikisha kwamba wana ujuzi wa mipango shirikishi, utekelezaji, usimamizi na tathmini, na mchango katika uchambuzi na uundaji wa sera.

5. Wakaguzi watasimamia mafunzo katika ngazi za wilaya na kata, kijiji na shule. Kutakuwa na ukaguzi wa shule kila baada ya miaka miwili kwa kiwango cha chini.
6. Wakuu wa shule watafanya kazi pamoja na kamati za shule kutunga na mara kwa mara kutengeneza upya mipango ya miaka mitatu ya maendeleo ya shule. Mipango hii itakuwa msingi wa maamuzi yote kuhusu maendeleo katika ubora na utoaji wa elimu, na ujenzi mpya katika shule.
7. Kamati za shule zitapewa mafunzo kuhusu wajibu na majukumu yake mapya.
8. Fedha zenye thamani sawa na dola za Kimarekani 500 kwa shule zitatolewa kwa ajili ya mafunzo ya Kamati ya shule. Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) pia zinaweza kuomba fedha hizo kwa utoaji wa mafunzo kama hayo.

3.3.3 Usimamizi wa Fedha

MMEM itahitaji baadhi ya taratibu mpya za fedha kuanzishwa ili kukabidhi usimamizi wa fedha katika ngazi ya shule. Walimu Wakuu, kamati za shule, Waratibu Elimu Kata, na wafanyakazi wa wilaya, mkoa na taifa watapata mafunzo katika mtindo mpya wa usimamizi wa fedha.

Mkazo wa mafunzo utakuwa katika uwezo wa kila ngazi katika mfumo unaosaidiwa na kanuni za fedha na kutoa taarifa nzuri katika matumizi ya Ruzuku ya kila mtoto na ya Maendeleo na ya Mfuko wa Kujenga Uwezo.

MALENGO

1. Kuanzisha taratibu za fedha na vielelezo ambavyo ni sehemu ya mpango.
2. Kuhakikisha usimamizi na matumizi mazuri ya fedha katika ngazi zote muhimu.

MIKAKATI

1. Mamlaka ya fedha kwa ajili ya kuinua ubora wa elimu katika ngazi ya shule yatahamishiwa katika ngazi ya shule. Shule zote zitafungua akaunti ya benki.

2. Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi utaanzisha utaratibu wa aina tatu wa fedha ambazo zitasaidia shule moja kwa moja: (a) Ruzuku kwa kila mtoto itatoa msaada kwa ajili ya kuinua kiwango cha ubora wa elimu (b) Ruzuku ya Maendeleo itasaidia katika ujenzi wa majengo mapya na (c) Mfuko wa kujenga Uwezo utatoa msaada kwa ajili ya mafunzo ya kamati ya shule.
3. Kamati za shule zitakuwa na uwezo wa kuongeza ruzuku hizi kutokana na misaada ya jumuia.
4. Taratibu na kanuni sahihi za hesabu, taarifa na ukaguzi wa fedha za MMEM utaanzishwa.
5. Vitabu vya mwongozo wa usimamizi wa fedha vitatolewa na mafunzo yatatolewa ambayo yataziwezesha kamati za shule na wasimamizi katika kila ngazi muhimu kuelewa na kutekeleza taratibu sahihi za fedha.
6. Dhana za uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya fedha za umma

   zitatiliwa mkazo katika mafunzo na taarifa zitatolewa katika ngazi zote za mfumo wa elimu, ikiwa ni pamoja na kwa wazazi na jumuiya.

3.3.4 Mfumo wa Usimamizi wa Habari wa Menejimenti ya Elimu

Mameneja na wanamipango wa elimu wanahitaji taarifa sahihi, kwa wakati muafaka itakayosaidia kufanya kazi inayofaa na kuendeleza mfumo wa elimu. Kipengele cha kibinadamu katika mahitaji haya ni kwamba katika mfumo wa ugawaji madaraka, washikadau wote wanapaswa kujiona kama wakusanyaji, watoaji na watumiaji wa taarifa za kielimu. Kipengele cha kiteknolojia ni kutumia kompyuta kama kifaa cha kuunda Mfumo wa Taarifa wa Menejimenti ya Elimu (EMIS) ambao unaweza kuandaa na kuweka data za kielimu katika muundo ambao utasaidia usimamizi, tathmini na mipango.

MALENGO

1. Kuhakikisha kwamba mameneja wa elimu katika ngazi zote wanaweza kuanzisha na kuwa na fursa ya kupata data za

uhakika na taarifa kuhusu mfumo wa elimu, ikiwa ni pamoja na takwimu za vifo vinavyotokana na UKIMWI.
2. Kuhakikisha kwamba mipango na sera ya elimu inazingatia taarifa mpya na zenye uhakika kutoka katika viashirio muhimu vyote.

MIKAKATI

1. Mfumo wa Usimamizi wa Habari wa Menejimenti ya Elimu (EMIS) utatengenezwa upya kujumuisha data zote muhimu za elimu.
2. Msaada wa nyongeza wa vifaa na teknolojia utatolewa na utaratibu ulioanzishwa ambao utahakikisha kuwepo kwa mtiririko wa habari na mawasiliano unaofaa
3. Mafunzo yatatolewa katika utawala na matumizi ya EMIS. Mkazo utakuwa katika wajibu wa mameneja na wanamipango katika ngazi zote kukutana na kutoa taarifa haraka kwa washikadau wakati wote wa mfumo.
4. Menejimenti ya kujenga uwezo itasisitiza wajibu wa washikadau katika kuhakikisha mtiririko unaofaa wa taarifa sahihi za kielimu.

3.4 MIFUMO YA TAASISI

Umuhimu wa nne wa kimkakati kwa elimu ya msingi ni kuyafanya kuwa bora matumizi ya rasilimali watu, vifaa na fedha ndani ya taasisi zilizopo ambazo zina mfumo wa elimu.

Ili kufikia lengo hili la kipengele cha watu na vifaa, MMEM itahitaji kiasi fulani cha marekebisho kitaasisi. Juhudi za Serikali kugawa madaraka zinategemea mabadiliko yote katika taasisi na wajibu na majukumu ya mtu binafsi.

Ili kufikia lengo hili la kipengele cha vifaa na fedha, Serikali itaongeza mgawanyo mzima wa bajeti ya elimu ya msingi na itahamasisha ushiriki mkubwa wa jumuiya na kuhimiza ufadhili wa pembejeo za fedha. Ndani ya bajeti ya MMEM pembejeo zisizotumia mshahara na uwiano wa matumizi ya kawaida utaongezeka.

3.4.1 Mipango ya Kiutawala

Wizara kuu husika zitaendelea kulenga katika sera ya

maendeleo na usimamizi. Kutakuwa na ongezeko la ugawaji wa mamlaka kwa serikali za mitaa na shule kusimamia utoaji wa elimu na maendeleo. Lengo la msingi ni kwa kila wilaya kuweza kutoa fursa sawa kwa watoto kwa kutoa huduma bora za elimu.

MALENGO

1. Kukamilisha upya mfuatano wa wajibu na majukumu miongoni mwa Mamlaka za Elimu za Mtaa, Wilaya na Serikali Kuu.
2. Kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa na vyombo vya Serikali za Mkoa zinasaidia kikamilifu katika utoaji wa elimu ya msingi kwa watoto wote.
3. Kuhakikisha kwamba wafanyakazi wazalendo wanashirikiana kikamilifu katika uendelezaji wa sera za elimu ya msingi.

MIKAKATI

1. Mpango unaeleza na kupanua wajibu na majukumu ya vyombo vya serikali za mitaa katika kuhakikisha elimu ya msingi inatolewa.
2. Katika ngazi za kijiji, kata, wilaya na mkoa ushirikiano mkubwa na mshikamano kati ya wafanyakazi wa elimu na walio katika sekta nyingine utaimarishwa.
3. Wafanyakazi wanaohusika na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi watabainishwa katika ngazi ya wizara, na miundo inayofaa kwa ajili ya uratibu ndani na katika wizara itaimarishwa au kuanzishwa.
4. Makatibu wakuu watawateua maafisa wakuu wawili kuwa Waratibu wa Programu ambao watasimamia utekelezaji wa MMEM.

3.4.2 Majukumu ya Taasisi zinazohusika na MMEM

- **Ngazi ya Kijiji/Mtaa/Kitongoji**

  Lengo la Serikali la kupanua demokrasia ya ushiriki na uwajibikaji katika ngazi zote litahitaji kujihusisha zaidi kwa wanaume, wanawake na watoto kutoka kwenye jumuiya. Ubia kati ya walimu, shule na jumuiya utaendelezwa ili kuimarisha usimamizi wa shule. Katika ngazi ya shule kuna Kamati ya shule ambayo inawajibika kwa Serikali ya Kijiji

katika Halmashauri za Wilaya na kwa kamati ya Mtaa katika Halmashauri za Mjini na Manispaa.

Kupitia utoaji wa raslimali za fedha na rasilimali watu, Serikali itatoa uwezo zaidi kwa kamati za shule kuwajibika kwa uongozi na maendeleo ya shule.

Majukumu ya Kamati ya Shule yatajumuisha:

1. Kuwaelimisha na kuwahusisha wanafunzi wote, wazazi na wafanyakazi wa shule kuhusu nafasi yao katika kuongeza faida ya elimu ya msingi.
2. Kusimamia masuala ya kila siku ya shule.
3. Kufanya kazi pamoja na Mwalimu Mkuu na walimu wengine katika kutayarisha Mpango kamili wa Maendeleo ya Shule.
4. Kupitisha Mipango kamili ya Maendeleo ya shule na bajeti na kuvikabidhi kwa kamati ya mtaa, au baraza la kijiji na baadaye katika kamati ya maendeleo ya kata na hatimaye katika Mamlaka za Serikali za Mtaa kwa ajili ya uratibu wa makini na uimarishaji, na kuwasilishwa kwa Sekretariati ya Mkoa .
5. Kuwezesha mipango, uwekaji bajeti na utekelezaji wa shughuli zinazogharimiwa na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi.
6. Kufungua akaunti benki na kusimamia kwa ufanisi na usahihi fedha zinazopokelewa kwa ajili ya utekelezaji, wakati huohuo kuhakikisha kunakuwepo na uwajibikaji na uwazi katika michakato iliyotumika, ikijumuisha kuweka wazi upatikanaji wa mapato na matumizi.
7. Kuhakikisha kunakuwepo na utunzaji mzuri wa mali zilizopatikana kutoka na fedha za MMEM.
8. Kutayarisha na kukabidhi ripoti sahihi ya maendeleo na fedha kwa muda muafaka kwa baraza la kijiji, kamati ya mtaa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.
9. Kuwasilisha ipasavyo taarifa za kielimu kwa wazazi wote, wanafunzi, washikadau wa jumuia, na kwa kijiji, kata/mtaa hadi ngazi ya Halmashauri.

- **Ngazi ya Kata**

  Inatarajiwa kwamba jumuiya na viongozi katika kata watashirikiana kuhakikisha kwamba watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa na kuhudhuria shuleni.

Mratibu wa Elimu Kata (MEK) atasimamia maendeleo ya shule za msingi katika shule zote zilizo ndani ya kata yake

Majukumu ya Mratibu Elimu Kata yatajumuisha:

1. Kuhakikisha kwamba wasichana na wavulana wote wenye umri wa kwenda shule katika kata wanaandikishwa na kuhudhuria shuleni ifikapo mwaka 2004.
2. Kubadilishana taarifa na kuwawezesha wazazi wote na sehemu kubwa ya jumuia kushiriki katika kutekeleza malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi.
3. Kusaidia kutambua vipaumbele kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya shule na kusaidia katika michakato ya mipango.
4. Kuhakikisha kwamba utekelezaji wa shughuli zinazogharimiwa na MMEM unafanywa na kamati za shule katika hali ya uwazi na uwajibikaji kwa kulinda na kuhimiza matumizi yanayofaa na usimamizi wa mfuko wa fedha.
5. Kuratibu mipango kamili ya Maendeleo ya Shule katika kata.
6. Kusambaza ipasavyo taarifa za elimu kwa shule na washikadau wenyeji.

Ngazi ya Halmashauri za Miji/Wilaya na Manispaa.

Mamlaka za Serikali za Mitaa itachukua jukumu zima la usimamizi na utoaji wa huduma zote za shule ya msingi ndani ya mipaka yake. Mipango ya ngazi ya baraza, uwezo wa uongozi na usimamizi utaimarishwa.

Sambamba na kanuni za kuboresha Serikali za Mitaa: mamlaka za wilaya na miji:

1. Zitajumuisha ushirikishwaji wenye maana wa washikadau wote wa jumuiya katika hatua za mipango, usimamizi na utekelezaji.

2. Katika hali ya ushirikishwaji na kwa pamoja zitatayarisha mipango ya maendeleo ya miaka mitatu na ya kila mwaka kwa ajili ya shule za msingi za wilaya.
3. Zitatumia mipango ya maendeleo kama msingi wa kutayarisha na kusimamia mahitaji ya Ruzuku ya Maendeleo kukabidhiwa katika shule.
4. Zitaongoza na kutekeleza matumizi yanayofaa na usimamizi wa mfuko wa fedha wa MMEM kwa kamati za shule, moja kwa moja na kupitia kwa kamati za maendeleo za kati na mabaraza ya kijiji.
5. Zitatengeneza na kuwasilisha ripoti za fedha za kila siku kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEM) na Wizara ya Elimu na Utamaduni kupitia Sekratariati ya Mkoa.
6. Zitatoa msaada wa kiufundi kwa kamati za shule na kijiji katika kazi ya uwakala, matumizi ya fedha na kutoa ripoti inayofaa na kwa muda muafaka.
7. Zitasimamia, kuhakiki na kutathmini mara kwa mara maendeleo ya shughuli za MMEM na kutoa ripoti katika Sekretarieti ya Mkoa kwa ajili ya kupelekwa kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Elimu na Utamaduni.
8. Zitawasilisha taarifa za kielimu ipasavyo kwa kijiji, kata, shule na makundi mengine ya washikadau wenyeji, pamoja na ngazi za kimkoa na kitaifa.

- **Ngazi ya Mkoa**

  Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya watazisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuweka mazingira yanayowezesha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa Sekretariati ya Mkoa itatoa msaada wa kiufundi na huduma ya ushauri kwa wilaya ili kuiwezesha kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi .

Majukumu ya Ofisi ya Elimu Mkoa kwa kuzingatia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ni:

1. Kufanya ukaguzi wa fedha wa ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Shule ili kuhakikisha kuwa malengo ya utendaji na taratibu za kifedha zinafuatwa.

2. Kuongoza, kuratibu na kusimamia utoaji wa elimu ya msingi unaofanywa na mamlaka za mtaa.
3. Kutoa msaada wa kiufundi katika ofisi za elimu za wilaya.
4. Kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatayarisha mipango imara ya miaka mitatu ya maendeleo ya elimu ambayo itaendana na sera ya elimu ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na kuhakikisha ubora wa viwango.
5. Kuimarisha mipango na bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa za elimu ya msingi ndani ya Mkoa na kuziwasilisha kwa Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu na Utamaduni ili kuwezesha kupitisha na kuwasilisha Hazina.
6. Kuwasilisha ipasavyo taarifa za kielimu kwa wilaya na washikadau wengine wenyeji.
7. Kuwasilisha ipasavyo taarifa na matatizo kutoka katika Wilaya na jumuiya kwenda katika ngazi ya kanda na taifa.

- **Wizara ya Elimu na Utamaduni**

  Wajibu na kazi za Wizara ya Elimu na Utamaduni ni pamoja na mipango shirikishi, usimamizi na tathmini; na uamuzi wa sera, viwango vya uhakiki bora. Katibu Mkuu atatoa mkakati mzima wa uongozi kwa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na maendeleo ndani ya Wizara ya Elimu na Utamaduni katika utekelezaji wa shughuli zake, Wizara ya Elimu na Utamaduni inasaidiwa na taasisi kuu za TIE, NECTA, MANTEP, IAE, TLS na UDSM.

  Afisa Mwandamizi atateuliwa kama Mratibu wa Programu ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) atakayekuwa na madaraka kwa Wakurugenzi wa Wizara ya Elimu na Utamaduni na kushauriana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs), wafadhili na washikadau wengine.

Kulingana na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) majukumu ya Wizara ya Elimu na Utamaduni ni:

1. Kutayarisha sera zitakazohakikisha elimu bora kwa wote Tanzania.

2. Kutayarisha katika hali ya kushirikiana mipango ya kina ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi.
3. Kufuatilia, kuhakiki na kutathmini maendeleo, matokeo na athari za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) kwa uhakika wa ubora, na kutoa ripoti za kawaida kama hizo kwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi.
4. Kutayarisha ripoti za kawaida za matumizi ya fedha za kuziwasilisha kwenye Mpango wa Maendeleo ya Msingi na Kamati ya uendeshaji.
5. Kushirikiana na Timu ya MMEM ya Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika masuala ya Mipango, Ufuatiliaji na tathmini.
6. Kushiriki kwa pamoja kama mshikadau katika mkutano wa mwaka wa maendeleo wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) wa kuhakiki sekta ya elimu pamoja na programu ya elimu ya msingi na isiyo rasmi.
7. Kusaidia na kujenga uwezo wa kitaaluma wa Ofisi za Elimu za Wilaya.
8. Kukusanya na kuwasilisha taarifa za elimu ikiwa ni pamoja na data zinazohusiana na UKIMWI katika mfumo wa ngazi zote, taasisi zinazotoa msaada kielimu na washikadau wanaopendelea jambo hili.
9. Kufanya ukaguzi wa shule kwa:

- Kufuatilia utoaji wa Elimu kama ilivyo katika mitaala iliyowekwa.
- Kuhakikisha kunakuwepo na ufanisi na ubora katika utoaji wa elimu.
- Kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi kwa kutathmini mafanikio ya elimu, kukuza maendeleo ya shule na kutoa ushauri kwa washikadau wote katika elimu.
- Kutoa mjibizo (feedback) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu na Utamaduni , kusaidia wakala wa elimu, wamiliki wa shule, mameneja na watawala katika ngazi zote.
- Kuhakikishwa kwamba kila shule inakaguliwa angalau kwa kiwango cha chini, kila baada ya miaka miwili.
- Kutoa ushauri kwa kamati za shule wa jinsi ya kusimamia uendeshaji wa shule ipasavyo na kidemokrasia.

- Kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kijiji, Mtaa, Kata na utawala wa shule katika kutoa ipasavyo na kwa ufanisi elimu bora ya msingi.
- Kuzishauri shule katika Mipango Kamili ya Maendeleo ya shule.
- Kuhakiki na kutathmini shughuli za MMEM na maendeleo kwa ujumla.
- Kukusanya na kuwasilisha taarifa za elimu kwa washikadau wote.

- **Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

  Jukumu la Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni kusimamia utoaji madaraka ya shughuli za serikali kwa ngazi ya wenyeji ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu ya msingi utakaofanywa na mamlaka za wilaya. Inatoa msaada wa kiufundi na ushauri kwa Sekretariati ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika ngazi ya taifa itatathmini na kuratibu mipango ya maendeleo ya elimu kimkoa ikisaidiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni.

  Timu ya MMEM ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaanzishwa ndani ya Ofisi na Afisa Mwandamizi/Mkuu atateuliwa kuwa Mratibu wa programu ya MMEM na atawajibika kuelekeza na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi.

Majukumu ya Timu ya MMEM ni:

1. Kukagua na kusimamia utoaji wa elimu ya msingi unaofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
2. Kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatayarisha mpango madhubuti wa miaka mitatu wa maendeleo ya elimu ambao unaendana na mipango ya maendeleo ya serikali na sera ya elimu ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na uthibitisho ya viwango bora.
3. Kuunganisha mipango na bajeti za Mkoa katika Mpango wa taifa wa utekelezaji ambao utaidhinisha uhawilishaji wa fedha za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi kutoka Hazina.
4. Kushirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni ili kusimamia, kuhakiki na kutathmini taarifa na matokeo ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi .

5. Kushiriki kama mshikadau mwenza katika mkutano wa mwaka wa Maendeleo wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESPD) wa kuhakiki programu ya elimu ya msingi na elimu isiyo rasmi.
6. Kusaidia na kujenga uwezo wa Sekretariati ya Mkoa (RS) na Mamlaka za Serikali za Mitaa .
7. Kuwasilisha taarifa za elimu kwa ngazi zote za mfumo na washikadau wanaopendelea suala hilo.
8. Kutoa taarifa za mara kwa mara za fedha na ripoti halisi kwa Hazina na Wizara ya Elimu na Utamaduni.

- **Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (BEDC)**

  Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi ni msingi mkubwa uliyopewa jukumu la kusimamia maendeleo ya elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu na elimu ya watu wazima na kuhakikisha inakamilisha malengo ya programu pana ya sekta ya maendeleo. Ndani ya muundo wa elimu ya msingi, BEDC ina mamlaka maalumu ya kulinda na kusimamia maendeleo katika elimu ya msingi. Kamati inaongozwa kwa pamoja na Makatibu Wakuu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Uanachama unajumuisha mwakilishi kutoka Wizara ya Fedha, Wakurugenzi muhimu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wawakilishi wa Mashiriki yasiyo ya Kiserikali, Chama cha Walimu na Wahisani hai katika elimu.

  Vikundi vya shughuli za kiufundi vinakutanishwa kama ni muhimu kwa vipengele maalumu vya maendeleo ya MMEM

  Pia Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi inaweza kutumia kazi kwa Kikosi cha Kazi (Task Force) cha BEDC chenye wawakilishi wa vikundi vyote wanachama muhimu.

Majukumu ya Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi kulingana na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ni:

1. Kuunda mipango ya elimu ya msingi inayoendana na sera ya serikali.
2. Kushirikiana na Mashirika ya Fedha na washikadau wengine katika kuunda na kusimamia fedha za shughuli zilizopangwa.

3. Kutambua mahitaji ya kiufundi na msaada wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa MMEM.
4. Kuratibu na kufuatilia usimamizi wa taarifa mbalimbali za habari za MMEM, Programu ya Habari, Elimu na Mawasiliano (IEC).
5. Kuchangisha rasilimali za Serikali na mhisani kupitia katika uanzishaji wa mfuko wa Programu ya Elimu (EPF) unaosimamiwa kama sehemu muhimu ya Akaunti imara ya Hazina katika Benki ya Tanzania.
6. Kuidhinisha ripoti ya fedha ya mwaka kuhusiana na bajeti na matumizi ya fedha za mpango, na kuchukua hatua ya ufuatiliaji unaofaa.
7. Kuhakiki kila mwaka viashirio muhimu vya utendaji kwa ajili ya kutathmini maendeleo ya MMEM na kuweka malengo kwa ajili ya mwaka mpya.
8. Kuanzisha na mara kwa mara kuhakiki utaratibu wa MMEM wa mipango, uongozi, usimamizi na tathmini, na ugharimiaji.
9. Kuhakikisha ushiriki wa washikadau katika shughuli ya mwaka ya Mchakato wa uhakiki wa ESDP na kusimamia vipengele vya elimu ya msingi na isiyo rasmi ya uhakiki wa jumla wa sekta ya elimu.
10. Kukusanya na kuwasilisha ipasavyo taarifa za kielimu kati ya wizara, wafadhili, NGOs na vikundi vingine vinavyowakilisha washikadau.

- **Kamati ya Uendeshaji ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu.**

  Matayarisho ya utaratibu katika nafasi ya kuratibu na kusimamia maendeleo ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu yatafanywa kusaidia utekelezaji wa programu ya sekta iliyo wazi. Hususan, Kamati ya Utendaji ya ESDP itaongoza na kuratibu mpango na utekelezaji wa awamu ya kwanza ya programu, na mpango wa vipengele vinavyofuata kwa Elimu ya Sekondari, Elimu ya Ualimu na Ufundi Stadi na Mafunzo na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (PMO) anaongoza kamati. Wajumbe wengine wa Kamati ni Makatibu Wakuu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni; Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,

Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo; Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto; Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafisishaji; na Fedha.

Wajibu wa Kamati umeainishwa kuwa ni:

1. Kusimamia utekelezaji, maendeleo na utimizaji wa maamuzi yanayohusiana na sera za elimu za taifa.
2. Kusimamia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu.
3. Kutoa kiwango cha juu cha uratibu kati ya wizara.
4. Kuhakikisha msimamo wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu unaendana na Sera za Serikali zilizo wazi.
5. Kuanzisha mpango wa mwaka wa pamoja wa washikadau wa uhakiki ambao utafanya kazi kwa kuingiliana na majukumu ya Serikali kwa michakato ya Mapitio ya Matumizi ya Umma (PER) na Makala Kuhusu Mkakati wa Kupunguza Umaskini (PRSP). Sekta ya uhakiki ya kila mwaka itaakisi na kupima masuala ya kiufundi yanayohusiana na ufanisi, matokeo mazuri na umuhimu wa programu katika sekta ya elimu, ikiwa ni pamoja na elimu ya msingi na elimu isiyo rasmi.

- **Wahisani na Mashirika ya Fedha**

  Aina mpya ya ushirikiano kati ya Serikali na jumuia ya wahisani imeanzishwa. Kanuni ya maendeleo ya sekta pana ya msaada ni kuimarisha mipango na mifumo iliyopo ya serikali kuliko kuanzisha jitihada za kipekee sambamba na mradi unaoendeshwa.

  Ongezeko kubwa la mwanzo katika msaada wa kifedha kutoka nje kuisaidia nchi kushughulikia ongezeko la uandikishaji mwaka 2002-2006 ni kipengele muhimu cha Mpango wa Elimu ya Msingi. Taratibu za kufuata muelekeo wa mhisani katika mipango ya Serikali zimeanzishwa kupitia Muundo wa Matumizi wa Muda wa kati na uhakiki wa Mapitio ya Matumizi ya Umma. Fedha za mhisani zilizotengwa kusaidia MMEM zitaongezwa katika zile za serikali katika “Mfuko” maalumu unaoitwa Mfuko wa Programu ya Elimu (EPF) au kupitia bajeti ya Serikali.

Kulingana na MMEM, majukumu ya mhisani ni:

1. Kufuata mipango ya muelekeo wa mhisani na msaada katika sera za Serikali, mipango na bajeti kwa ajili ya maendeleo na msaada wa elimu ya msingi.
2. Kuchangia mfuko wa msaada wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi, na kukubaliana na serikali kuhusu vigezo na sheria za kuhawilisha na kutoa fedha za Mpango wa Elimu ya Msingi zilizowekwa kwa pamoja katika Mfuko wa Programu ya Elimu .
3. Kuhakikisha kwamba mipango ya miradi yoyote ya elimu ya msingi isiyo ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi inakuwa ndani ya Makala ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini, Programu ya Maeneleo ya Sekta ya Elimu na ya Sera ya maendeleo ya Elimu ya Msingi.
4. Kushiriki kama ushirika wa washikadau katika shughuli ya mwaka ya uhakiki wa ESDP wa sekta ya elimu ukijumuisha programu za elimu ya msingi na elimu isiyo rasmi.
5. Kuwasilisha ipasavyo taarifa kwa wizara na kwa washikadau wengine wa taifa, na katika hali ya uwazi wakati wote.

- **Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Jamii**

  Sera ya Serikali ya kutoa elimu ya msingi yenye ubora wa hali ya juu kwa watoto wote inahitaji ushiriki wa safu kubwa ya watendaji. Vyama visivyo vya kiserikali na jumuia nyingine za jamii zina wajibu muhimu wa kufanya katika jitihada hizi.

Kulingana na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi, majukumu ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Jumuia nyingine za jamii ni:

1. Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mipango, utekelezaji na usimamizi katika ngazi zote zinazounga mkono malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu
2. Kushiriki kama ushirika wa washikadau katika Mpango wa mwaka ya uhakiki wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu, ikijumuisha programu za elimu ya msingi na elimu iliyo nje ya mfumo rasmi wa elimu.

3. Kuchangia uzoefu na maarifa yao, ikiwa ni pamoja na rasilimali watu, ufundi, fedha na vifaa kwa ajili ya uboreshaji na utoaji wa elimu ya msingi.
4. Kushirikishana habari na kuwezesha ushiriki wa jumuiya unaofaa katika elimu ya msingi na elimu isiyo rasmi.
5. Kukusanya na kuwasilisha taarifa za kielimu kutoka na kwenda katika shule, jumuiya, serikali na washikadau wengine.
6. Kuongoza uchambuzi na utetezi wa sera ya elimu.

4. BAJETI

Bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi inaakisi matumizi makubwa ambayo yataongezeka wakati mfumo unashughulikia kusambaa kwa uandikishaji. Mishahara ya walimu, elimu ya ualimu na Ruzuku kwa kila mtoto kitakuwa ni kipengele kikubwa chini ya matumizi ya kawaida, wakati ambapo Ruzuku ya Maendeleo itakayotumika kwa ujenzi na kuinua uwezo itatawala maendeleo ya matumizi katika kipindi cha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi.

Usanifishaji wa gharama za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi na mihtasari ya rasilimali imejikita katika baadhi ya dhana muhimu. Jambo muhimu katika hizo ni kwamba Zao Ghafi la Ndani ya Nchi (GDP) inategemewa kukua kwa kiwango cha asilimia 6, ikitoa ongezeko lisilobadilika

katika kiasi cha pato la ndani ambapo serikali inapanga bajeti za sekta. Jambo la pili muhimu ni kiasi cha fedha kutoka nje zinazotegemewa kama sehemu ya jumla ya rasilimali maalum Chanzo cha msingi cha fedha kutoka nje kitakuwa ni bajeti ya juhudi za kusaidia bajeti ya kupunguza umaskini, wakati ambapo pembejeo muhimu ya pili itatoka katika juhudi za kupunguza deni kwa Nchi Maskini zenye Madeni Makubwa (HIPC).

Kutokana na jumla hii ya rasilimali maalum Serikali itachukua hatua ya kutenga mpaka asilimia 25 ya matumizi yake ya kawaida katika sekta ya elimu. Ndani ya Hisa ya jumla ya elimu, asilimia 62 zitatengwa kwa elimu ya msingi.

Mwanzo wa MMEM pengo la fedha kati ya rasilimali zilizopo na gharama zilizokadiriwa zinaweza kuwa kubwa sana, lakini kadri siku zinavyokwenda pengo linategemewa kuwa dogo. Serikali itaendelea kujadiliana ili kupata mchango

mkubwa wa fedha kutoka kwa jumuia wahisani kwa ajili ya gharama za matumizi ya kawaida na za maendeleo ya MMEM. Kwa kuongezea, michango ya hiyari ya jumuia itaendelea kuimarishwa na kuendeleza maendelezo ya lazima, kama vile utoaji wa vyakula kwa ajili ya juhudi za kulisha shule.

Jedwali hapo chini linaonyesha matumizi ya kawaida, maendeleo na jumla ya bajeti ya MMEM kwa kila mwaka kwa miaka mitano. Maelezo zaidi ya tarakimu hizi yanaweza kupatikana katika viambatisho.

Jedwali 1: Muhtasari wa gharama za MMEM

Gharama (T.sh.Milioni)	2002	2003	2004	2005	2006
Gharama za matumizi ya kawaida	199,831.6	234,774.8	271,989.2	296,292.2	312,642.5
Gharama za Maendeleo	99,633.0	88,274.0	92,424.0	48,330.0	43,608.0
Jumla ya gharama za MMEM	299,464.6	323,0.48.8	364,413.2	344,622.2	356,250.5

KIAMBATISHO 1: BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA YA ELIMU YA MSINGI – GHARAMA ZA MTU MMOJA

Kipengee cha Bajeti	**Vigezo Vikuu**	**2002**	**2003**	**2004**	**2005**	**2006**
A. NGAZI YA SHULE						
1. MISHAHARA wa mwalimu	Ongezeko la Mshahara	20633.74	20266.92	19837.73	20631.24	21456.49
	Ongezeko la Mshahara Walimu	4.00%	4.00%	4.00%	4.00%	4.00%
	PTR Muhimu	50.00	52.94	56.25	56.25	56.25
	Ziada ya shifti mbili	917.06	1430.61	1983.77	2063.19	1072.820.4
	% D/S Walimu	0.11	0.18	0.25	0.25	0.25
Jumla Ndogo ya Mishahara		**21550.79**	**21697.52**	**21821.51**	**22694.43**	**22529.31**
2. GHARAMA ZA UENDESHAJI	Ruzuku kwa kila mtoto (US $ 10) $ 1 = Tsh. 900	9000.00	9000.00	9000.00	9000.00	9000.00
	Mitihani	573.84	497.77	453.72	593.55	629.77
	% ya kuandikisha darasa la 4	0.13	0.12	0.11	0.18	0.19
	% ya kuandikisha darasa la 7	0.11	0.09	0.08	0.08	0.08
	Ustawi wa Wanafunzi	301.93	301.93	301.93	301.93	301.93
	Kukua kwa ustawi wa wanafunzi	0.00%	0.00%	0.00%	0.00%	0.00%
	JN ya Gharama za U	9875.77	9799.7	9755.65	9895.48	9931.70
Jumla Ndogo Kiwango cha Shule		**31,426.57**	**31,997.22**	**31,577.16**	**32,589.91**	**32,461.01**

A. UKAGUZI						
1. MISHAHARA		100.83	99.04	96.94	100.82	104.85
	Ongezeko la Mshahara wa Mkaguzi	4.00%	4.00%	4.00%	4.00%	4.00%
	Idadi ya walimu kwa Kila mkaguzi	211	211	211	211	211
	GHARAMA ZAUENDESHAJI	73.01	73.01	73.01	73.1	73.01
	Kiwango cha ongezeko la gharama za uendeshaji	0.00%	0.00%	0.00%	0.00%	0.00%
Jumla ndogo ya Usimamizi		173.84	172.05	169.95	173.83	177.86
TAWALA ZA MKOA NA WILAYA	1. MISHAHARA	557.41	561.21	564.41	586.99	610.47
	%JN ya mshahara wa shule	2.59%	2.59%	2.59%	2.59%	2.59%
	2.GHARAMA ZA UENDESHAJI(GU)	2,548.97	2,548.97	2,548.97	2,548.97	2,548.97
	Ongezeko la GU	48.26%	0.00%	0.00%	0.00%	0.00%
3 MAFUNZO KAZINI	(MK)	107.54	107.54	107.54	107.54	107.54
	Ongezeko la MK	0.05%	0.00%	0.00%	0.00%	0.00%
Jumla ndogo ya ongezeko la U wa M/W		**3,213.92**	**3,217.72**	**3,220.92**	**3,243.50**	**3,266.98**
A. UTAWALA WA TAIFA (UT)						
	1. MISHAHARA	94.78	95.43	95.97	99.81	103.81
	% ya JN ya mshahara wa Shule	0.44%	0.44%	0.44%	0.44%	0.44%
	2. GHARAMA ZA UENDESHAJI (GU)	496.25	496.25	496.25	496.25	496.25
	Ongezeko la GU	0.00%	0.00%	0.00%	0.00%	0.00%
Jumla ndogo ya Ongezeko la UT		591.03	591.68	592.22	596.06	600.05
A. ELIMU YA UALIMU NA MTAALA (EU/M)						
1. KUAJIRI WALIMU WAPYA	1. Gharama za Wanaoanza kazi	418.46	466.22	371.74	245.44	235.05
	2. MAFUNZO KAZINI	518.03	448.17	392.96	377.30	363.15
	3. KUKUZA MTAALA	203,51	80.03	70.17	63.37	64.85
Jumla Ndogo ya EU/M		**1140.00**	**994.42**	**834.87**	**686.11**	**663.05**
JUMLA YA GHARAMA YA MTOTO MMOJA Elimu Rasmi		36545.35	36473.08	36395.12	37289.41	37168,95

KIAMBATISHO 2: MUHTASARI WA GHARAMA ZA MMEM

		2002	**2003**	**2004**	**2005**	**2006**
Mipango ya uandikishaji Elimu ya msingi		36,545.35	6,247,624	36,395.12	37,289.41	37,168.95
	A.GHARAMA ZA KAWAIDA (Tsh. Milioni)	5,407,070	6,247,624	7,125,416	7,421,234	7,710,240
	Gharama za kawaida za Elimu ya msingi	197,530.0	227,870.0	259,330.4	276,733.4	286,581.5
	Gharama za kawaida za NFE.	2,301.6	6,904.8	12,658.8	19,558.8	26,061.0
JUMLA ya matumizi		**199,831.6**	**234,774.8**	**271,989.2**	**296,292.2**	**312,642.5**
A. GHARAMA ZA MAENDELEO						
UJENZI						
	Madarasa	57,551	55,594	58,942	28,197	24,205
	Usafi na Maji	7.000	7,000	7,000	--	--
	Nyumba za walimu	12,086	11,675	12,378	5,921	5,083
	Jumla ya G ya Ujenzi	76,637	74,269	78,320	34,118	29,288
KUJENGA UWEZO	Kujenga uwezo	5,337	5,436	5,535	5,643	5,751
	Kamati ya Shule	4,731	4,731	4,731	4,731	4,731
	Wilaya	830	830	830	830	830
	Mkoa	1,660	1,660	1,660	1,660	1,660
	Wizara	448	448	448	448	448
	Msaada wa kiufundi	13,006	13,105	13,204	13,312	13,420
	JN ya Kujenga Uwezo	2,000	900	900	900	900
	IEC	7,990	--	--	--	--
	UPANGAJI WALIMU	99,633.0	88,274.0	92,424.0	48,330.0	43,608.0
	JUMLA MMEM	**299,464.6**	**323,048.8**	**364,413.2**	**344,622.2**	**356,250.5**

KIAMBATISHO 3: UGHARIMIAJI MMEM

Jedwali 1: Muhtasari wa Rasilimali

Rasilimali	**2002**	**2003**	**2004**	**2005**	**2006**
GDP (Tsh. Milioni)	8,011,395	8,492,079	9,001,604	9,541,700	10,114.202
Kiwango cha Ukuaji	0.06%	0.06%	0.06%	0.06%	0.06%
Kiwango cha Kodi ya ziada	0.13%	0.13%			
Ushuru wa ndani	906,671	1,069,732	1,134,914	1,240,421	1,314,846
Msaada wa bajeti ya kupunguza Umaskini	182,429	241,058	228,564	228,564	228,564
HIPC	55,264	54,952	52,846	50,330	47,933
Jumla ya Fungu la Bajeti	1,144,364	1,365,743	1,416,325	1,416,325	1,591,344
Fungu la Matumizi ya kawaida	1,092,239	1,307,495	1,368,318	1,380917	1,551,560
Matumizi ya kawaida ya Elimu kama asilimia ya matumizi ya Jumla	25.00%	25.00%	25.00%	25.00%	5.00%
Elimu ya Msingi kama asilimia ya Jumla ya Bajeti ya kawaida ya elimu	62.00%	62.00%	62.00%	62.00%	62.00%
Mgawo wa Bajeti ya gharama za Kawaida ya Elimu	169,297	202,662	212,089	214,042	240,492

Jedwali 2: Pengo la Ugharimiaji

Gharama katika Tsh. Milioni)	2002	2003	2004	2005	2006
Gharama za Kawaida	199,831.6	234,774.8	271,989.2	296,292.2	312,642.5
Gharama za Maendeleo	99,633.0	88,274.0	92,424.0	48,330.0	43,608.0
Jumla ya gharama za MMEM	299,464.6	323,048.8	364,413.2	344,622.2	356,250.5
Jumla ya bajeti ya kawaida	169,270	202,662	212,089	214,042	240,492
Jumla ya bajeti ya Maendeleo	99,633.0	88,274	92,424	48,330	43,608
Jumla ya Rasilimali	268,930	290,936	304,513	262,372	284,100
Pengo la fedha za matumizi ya kawaida	30,534.6	32,112.8	59.900.2	82,250.2	72,150.5
Pengo la fedha za Maendeleo	99,633.0	88,274.0	92,424.0	48,330.0	43,608.0
Jumla ya pengo la fedha za MMEM	130,167.6	120,386.8	152,324.2	130,580.2	115,758.5
(Gharama katika Dola Milioni za Kimarekani)[5]					
Pengo la matumizi ya kawaida USD	34	36	67	91	89
Pengo la Maendeleo USD	110	98	102	54	48
Jumla ya Pengo la Fedha	144	134	169	145	129

KIAMBATANISHO 4: IDADI YA UANDIKISHAJI SHULE YA MSINGI

Jedwali 1: Jumla ya Matarajio ya Uandikishaji

	2001	2002	2003	2004	2005	2006
Wote wenye miaka 7	951,295	973,175	995,558	1,018,455	1,041,880	1,065,843
4% ya wenye umri wa miaka saba	38,052	38,927	39,822	40,738	41,675	42,634
Shabaha ya Ingizo jipya	809,182	1,500,000	1,600,000	1,640,969	1,041,880	1,065,843
Darasa la 1	110,312	1,486,053	1,604,759	1,648,374	1,049,656	1,054,699
Darasa la 2	753,885	801,683	1,412,259	1,543,652	1,588,768	1,032,298
Darasa la 3	692,037	735,271	781,859	1,354,233	1,502,712	1,551,532
Darasa la 4	632,911	679,098	721,719	767,425	1,301,239	1,469,988
Darasa la 5	553,389	567,762	604,953	643,008	737,435	1,230,629
Darasa la 6	584,156	554,063	566,604	602,699	640,632	732,53
Darasa la 7	526,205	581,142	555,471	566,025	600,792	638,560
Uandikishaji	3,852,875	5,405.070	6,247,624	7,125,416	7,421,134	7,710,240
Idadi ya 7-13	5,679,676	5,810,309	5,943,946	6,080,657	6,220,512	6,363,583
GER	0.85	0.93	1.05	1.17	1.19	1.21

Jedwali 2: Darasa la Kwanza: Matarajio ya Maingizo Mapya

Umri	2002	2003	2004	2005	2006
7	973,175	995,558	1,018,455	1,041,880	1,065,843
8	526,825	0	0		
9	0	256,260	0		
10	0	348,182	0		
11	0	0	221,266		
12	0	0	401,248		

Jedwali 2: Darasa la Kwanza: Matarajio ya Uandikishaji Mpya

Umri	2002	2003	2004	2005	2006
7	973,175	995,558	1,018,455	**1,041,880**	**1,065,843**
8	526,825				
9		256,260			
10		348,182			
11			221,266		
12			401,248		
Jumla	**1,500,000**	**1,600,000**	**1,640,969**	**1,041,880**	**1,065,843**

KIAMBATISHO 5: MAHITAJI YA MWALIMU NA DARASA

Jedwali 1: Mipango ya Mahitaji ya Mwalimu

	2002	2003	2004	2005	2006
Idadi ya vipindi vya kufundisha (vinavyohitajika)	120.113	138,836	158,343	164,916	171,339
% ya vipindi vya kufundisha kwa shifti 2	0.10	0.15	0.20	0.20	0.20
% Vipindi halisi vya kufundisha kwa shifti mbili	0.11	0.18	0.25	0.25	0.25
PTR[6]	50.00	52.94	56.25	56.25	56.25
Mahitaji ya Mwalimu	108,101	118,011	126,674	131,933	137,071
Upungufu 1.60%	1,611	1,730	1,888	2,027	2,111
Mahitaji ya ajira mpya	9,047	11,651	10,563	7,286	7,249

Jedwali 2: Matarajio ya Mahitaji ya darasa

	2002	2003	2004	2005	2006
Idadi ya nafasi za kufundisha inayohitajika	120,113	138,836	158,343	164,916	171,339
% nafasi za kufundisha zilizopatikana kwa shifti mbili	0.4	0.4	0.4	0.4	0.4
% ya madarasa ya shifti mbili	0.67	0.67	0.67	0.67	0.67
Mahitaji ya darasa	72,068	83,302	95,006	98,950	102,803
Madarasa yaliyokuwepo mwaka uliopita	60,000	72,068	83,302	95,006	98,950
Idadi ya uchakavu	0.03	0.03	0.03	0.03	0.02
Ujenzi mpya	12,068	11,234	11,704	3,944	3,853
Jumla ya ujenzi unaotakiwa	**13,868**	**13,396**	**14,203**	**6,794**	**5,832**

[6] Viwango vya PTR vinafikia kilele ifikapo 2004, na vinategemewa kushuka baada ya 2006

KIAMBATISHO 6: GHARAMA ZA MWANAFUNZI MMOJA SHULE YA MSINGI

Jedwali 1: Ruzuku ya mtu mmoja na Gharama nyingine za Kuinua Ubora

Gharama za Ruzuku ya mtoto mmoja	**USD**
Kukarabati vifaa	2
Vitabu vya kiada, miongozo ya kufundishia, vifaa vya kusoma vya ziada	4
Chaki, madaftari, kalamu za wino, penseli	2
Vifaa vya utawala	1
Karatasi za mtihani – kununua na kuchapisha	1
Jumla ya Ruzuku ya mtoto mmoja	**10**

Gharama nyingine	**USD**
Mtihani wa darasa la 4 (gharama ya kila mwanafunzi kwa wale tu wanaohudhuria darasa la IV)	**2**
Mtihani wa darasa la 7 (gharama ya kila mwanafunzi kwa wale tu wanaohudhuria darasa la VII)	**2**
Mafunzo ya ualimu kazini (33,200 kwa mwalimu kwa mwaka)	**40**
Mafunzo ya kamati ya shule (makadirio kwa shule)	500

Jedwali 2: Gharama za mtoto mmoja kwa shule ya msingi

Ngazi ya shule (Gharama ya mtu mmoja)	**T.sh**
Mishahara ya mwalimu	24,616
Vifaa vya kujifunzia	606
Bweni	269
Usafiri wa mwanafunzi	33
Ukaguzi	
Mishahara	120
Gharama za uendeshaji	73
Uongozi wa Mkoa na Wilaya	
Mishahara	637
Gharama za Uendeshaji	1,719
Mafunzo kazini	108
Uongozi wa Taifa	
Mishahara	108
Gharama za Uendeshaji	496
Jumla ya mchango wa serikali kwa mwanafunzi mmoja	28,785
Ruzuku kwa mahitaji binafsi ya mwanafunzi	193
Ongezeko la Gharama ya mwanafunzi mmoja	28,736

Chanzo: Galabawa (2000) Ripoti ya Hali ya Elimu ya Msingi

KIAMBATISHO 7: WATOTO NA VIJANA WALIO NJE YA MFUMO RASMI WA SHULE

Jedwali 1: Matarajio ya Mpango wa Taifa kwa utoaji Elimu kwa watoto na vijana wasio soma 2002 – 2006

	2002	**2003**	**2004**	**2005**	**2006**
Wilaya	40	80	100	113	113
Idadi ya vituo	1,000	3,000	5,5000	8,500	11,325
Idadi ya waandikishwaji wapya	80,000	160,000	200,000	240,000	226,000
Idadi ya waalimu wenye taaluma	660	1,980	3,630	5,630	7,494
Idadi ya wasaidizi wenye taaluma	1,340	4,020	7,370	11.370	15,156
Jumla ya lengo la uandikishaji (Miaka 10 – 13+)	**80,000**	**240,000**	**440,000**	**680,000**	**906,000**

Jedwali 2a: Makadirio ya Gharama ya Mtoto mmoja ya NFE kwa watoto na vijana walio nje ya mfumo rasmi wa shule

KIPENGELE	GHARAMA ZA MWAKA (Tsh.)	IDADI
Mshahara wa Mwalimu mwenye taaluma	540,000	kwa kila Mwalimu
Gharama za jumuia kwa wasaidizi wenye taaluma	240,000	kwa kila Msaidizi
Vifaa vya kujifunzia	4,500	kwa kila Mwanafunz
Mafunzo ya Msaidizi	180,000	kwa kila Kituo
Usimamizi na Tathmini	90,000	kwa kila Kituo
Msaada Ngazi ya Wilaya	180,000	kwa kila Kituo
Gharama za Uongozi wa NGO	180,000	kwa kila Kituo

Jedwali 2b: Makadirio ya Gharama za jumla za programu ya NFE

MWAKA	**2002**	**2003**	**2004**	**2005**	**2006**	**JUMLA YA GHARAMA**
Idadi ya Vituo	1,000	3,000	5,500	8,500	11,325	
Idadi ya wanafunzi	80,000	240,000	440,000	680,000	906,000	
Gharama za Bajeti	1,080,0	3,240.0	5,940.0	9,180.0	12,231.0	31,671
Gharama za GoT*	**Gharama za GoT ni mishahara ya Walimu wenye Taaluma.**					
Gharama za Jumuia	321.6	964.8	1,768.8	2,728.8	3,637.4	9,421.4
Vifaa	360.0	1,080.0	1,980.0	3,060.0	4.077.0	10,557.0
Mafunzo ya Wasimamizi	180.0	540.0	990.0	1,530.0	2,038.5	5,278.5
Usimamizi & Tathmini	90.0	270.0	495.0	765.0	1,019.3	2,278.5
Msaada wa Wilaya	90.0	270.0	495.0	765.0	1,019.3	2,278.5
Gharama za Uongozi wa NGO	180.0	540.0	990.0	1,530.0	2,032.5	5,278.5
Jumla ya Gharama ya mwaka	**2,301.6**	**6,904.8**	**12,658.8**	**19,558.0**	**26,061.0**	**67485.0**

***Gharama za GoT ni mishahara ya Walimu wenye Taaluma $ 1 = Tsh. 900.**

KIAMBATISHO 8: MUUNDO WA KITAASISI WA ESDP KWA UTEKELEZAJI WA MMEM